AgriSpatial
LIMA NASI EPUKA HASARA

# Huduma na Gharama za AgriSpatial

**Dhamira Yetu**

Kuwawezesha wakulima kutumia teknolojia ya kisasa ya mifumo ya taarifa za kijiografia na utambuzi wa mbali. kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi yanayo ongozwa na takwimu za kisayansi. Tunashirikiana na wataalamu wa kilimo kubaini mahitaji ya mazao, kuchambua picha za anga, kufuatilia afya ya mimea, hali ya hewa na kuainisha maeneo bora kwa kilimo cha mazao mbalimbali. Ili kufanikisha haya, tunashirikiana na vyuo vinavyotoa elimu ya "GIS, Remote Sensing" na kilimo ili kupanda mbegu ya uelewa wa teknolojia ya anga kwa wataalamu wa kilimo wa sasa na wa baadaye. Tunashirikiana na vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii katika kutoa elimu pia tunalenga kushirikiana na taasisi za serikali chini ya Wizara ya Kilimo ili kuifikia jamii pana ya wakulima Tanzania.

**Dira Yetu**

Kuleta mapinduzi ya kweli kwenye kilimo kwa kuhakikisha kila mkulima nchini Tanzania bila kujali ukubwa wa shamba anapata fursa ya kutumia taarifa za kijiografia katika kufanya maamuzi ya kilimo kupitia teknolojia ya Mifumo ya taarifa za kijografia na utambuzi wa mbali (GIS & Remote Sensing). Tunatamani kuona kilimo chenye tija, kinacho linda mazingira na kustahimili mabadiliko ya tabianchi na kuchangia usalama wa chakula kwa taifa na dunia kwa ujumla.

## 1. Fahamu Kuhusu AgriSpatial

AgriSpatial ni kampuni ya teknolojia ya kilimo inayolenga matumizi ya data za Kijografia kulingana nae neo husika kupitia picha za setilaiti na uchunguzi wa kutumia drone ili kutoa suluhisho za kilimo cha usahihi. Tunatumia utambuzi wa mbali kupitia satelaiti kuunda mikakati ya kilimo chenye maarifa ya ndani kwa ajili ya kilimo endelevu na rafiki kwa mazigira.

Huduma zetu kuu ni pamoja na:

- Ramani za Mipaka ya Mashamba na Uchunguzi Mazingira Asilia ya Eneo la shamba.
- Utambuzi wa topografia ya eneo (DEMs)

- Uchambuzi wa Hali ya Hewa kwa Muda Mrefu
- Uchambuzi wa Maeneo bora na sahihi kwa kilimo kulingana na aina ya zao
- Ufuatiliaji wa Afya na ukuaji wa Mazao
- Makadirio ya Mavuno
- Uchambuzi wa Mtiririko wa Maji
- Uchambuzi wa Uwezekano wa uwepo wa Maji ya Chini Ardhi
- Ripoti na Mapendekezo ya Kitaalamu.

## 2. Vifurushi/Aina za huduma

**Bei za kila kifurushi**

| Kifurushi | Huduma zinazotolea | Bei (USD) | Bei (TZS) | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| **Starter** | • Ramani ya Mipaka ya Shamba(Maji ya nukta ya eneo,ukubwa wa shamba n.k)<br>• Uchunguzi wa maeneo yenye ustawi bora wa mazao(kutambua maeneo gani yanafaa kulimwa zao gani).<br>• Uchambuzi wa Hali ya Hewa kwa miaka 10 nyuma au zaidi(kuepuka Athari za Mabadiliko ya tabia nchi). | $700 | TZS 1,820,000 | Wakulima wapya au wawekezaji wanaoanza kilimo cha teknolojia |
| **Standard** | • Huduma zote zilizopo Starter +uchunguzi wa aina mbali mbali za Udongo & uchunguzi wa topografia kutambua miinuko na mabonde katika shamba, Uchambuzi wa Mtiririko wa Maji, Ufuatiliaji wa Afya na ukuaji wa Mazao. | $1,500 | TZS 3,900,000 | Mashamba yanayo milikiwa na vyama vya ushirika. |
| **Premium** | • Huduma zote za Standard + Makadirio ya Mavuno.<br>• Uchambuzi wa maeneo yenye Maji ya Chini ya Ardhi (kurahisisha uchimbaji wa visima)<br>• Msaada Maalum wa Kiufundi, Ratiba ya kuanza kilimo n.k | $2,500 | TZS 6,500,000 | Mashamba makubwa, biashara za kilimo, NGOs,ushirika mkubwa. |

## 3. Namna Tunavyotoa Huduma

**Awamu ya 1**

- Ukusanyaji wa Data ya Anga na Uchunguzi wa Shambani
- Tunakusanya data zilizopo: picha za setilaiti, DEMs, data za udongo, na hali ya hewa ya muda mrefu.
- Tunafanya uchunguzi wa ardhini kwa kutumia GPS na drone.

**Awamu ya 2**

- Uchambuzi wa Anga na Upangaji wa Shamba
- Tunachambua ufaafu wa mazao kwa kutumia data za hali ya hewa, udongo na mwinuko.
- Tunatengeneza DEMs kwa ajili ya mtiririko wa maji.
- Tunatathmini uwezekano wa maji ya chini ya ardhi.
- Tunapanga mpangilio bora wa shamba.
- Tunafuatilia afya ya mimea kwa picha za setilaiti za wakati halisi.

**Awamu ya 3**

- Ripoti na Mapendekezo ya Kitaalamu
- Tunatayarisha ripoti ya kina yenye ramani na uchambuzi wote.
- Tunatoa mapendekezo maalum kuhusu mazao, usimamizi wa shamba, na matumizi ya pembejeo.
- Tunawasilisha Mpango Mkuu wa Shamba kwa mteja kwa maoni na utekelezaji.

## 4. Viambatanisho(Deliverables)

1. Ramani ya Mipaka ya Shamba
2. Ramani ya Uchunguzi wa Anga na Muinuko wa Ardhi
3. Ripoti ya Mtiririko wa Maji
4. Ripoti ya maeneo yenye uwepo wa Maji ya Chini ya Ardhi
5. Ripoti ya aina na hali ya Udongo
6. Ramani inayoonesha maeneo yenye uzalishaji mzuri kulingana na aina ya zao la mteja.
7. Ramani na Ripoti ya Afya na Maendeleo ya ukuaji wa Mazao na maeneo yaliyopo kwenye Hatari.

### 5. Muda wa Kukabidhi Kazi

Huduma nyingi zitakamilika ndani ya wiki 2 hadi 3 baada ya ukusanyaji wa data, kulingana na ukubwa wa shamba, hali ya hewa, na ugumu wa eneo.

### 6. Masharti

- Malipo kwa awamu mbili:
    - 25% kabla ya kuanza
    - 75% baada ya kukamilika
- Hati, ramani na ripoti zitamilikiwa na AgriSpatial hadi malipo yawe kamili.
- Kazi ya ziada au marekebisho nje ya makubaliano yatatozwa kwa makubaliano ya pande zote.

### 7.Ahadi Yetu

AgriSpatial imejikita katika kuleta mapinduzi ya kilimo kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya matumizi ya Mifumo Taarifa za Kijografia na Utambuzi wa Mbali ili kuhakikisha wakulima wanaongeza tija, kupunguza gharama na kupata mavuno ya uhakika.